**Ndugu yangu mpendwa! Hongera sana kwa kuokoka!** Sasa umekuwa mtoto wa Mungu kamili. "*Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.* ***Yohana 1:12.***"

Mbingu zinafurahi kwa  uamuzi wako. Sasa ili uendelee kukua katika uhusiano huu mpya, naomba ufanye mambo haya matatu muhimu.

- **Jambo la kwanza**; Soma Neno la Mungu kila siku. Biblia ni chakula cha roho yako kinachokupa nguvu ya kushinda majaribu kila siku. ***Zaburi 119:11***.

- **Jambo la pili**; Omba bila kukoma. Boresha uhusiano wako na Mungu kwa kuzungumza naye wakati wote kama rafiki na baba yako. ***1Watesalonike 5:17 - 18.***

- **Jambo la tatu**; tafuta kanisa la kiroho. Shirikiana na waamini wengine ili upate maarifa na kukua katika imani kwa usahihi. ***Waebrania 10:25.***

---

**Sisi tunapatikana Kanisa la
T.A.G Mwenge Christian Centre Dar es Salaam.**

**Na kama ungependa kupata msaada zaidi wa jinsi ya kuanza safari yako na Mungu, tafadhali tupigie au tutumie ujumbe mfupi wa maandishi kwa namba 0713 250034. (*Mkurugenzi wa uinjilisti na umisheni Mwenge Christian Center)*. Mungu akubariki sana. Amen.**

Imetayarishwa na kuchapishwa **ROM MEDIA Gospel Campaign** +255 713 310721.

## KIZUIZI KIMEONDOKA

# YESU NI DARAJA!

*Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza, mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo.*
***Waefeso 2:13-19***



# PAZIA LIMEPASUKA, KIZUIZI KIMEONDOLEWA

Hapo mwanzo palikuwa na umbali mrefu kati ya mwanadamu na Mungu. Katika nyakati za agano la kale uhusiano wetu na Mungu ulipitia kwa makuhani na mfumo wa hekalu. Tunasoma hii kwenye kitabu cha ***Kutoka 28 :1. Waefeso 2: 13 -20, Mathayo 27:51.***

Watu walimheshimu sana Mungu, lakini walikuwa bado wakitenganishwa naye na pazia lililoashiria kuwa dhambi imeweka ukuta kati ya Mungu na wanadamu. Ingawa walimwabudu, kulikuwa na umbali uliowazuia wasimjie Mungu kwa ukaribu. Lakini ashukuriwe Mungu kwa upendo wake, akaleta suluhisho la kudumu la tatizo lile. Mungu hakutaka kabisa uendelee kukaa mbali naye. Hivyo aliona hitaji la moyo wako na akaamua kuchukua hatua ya kwanza kwa kumtoa mwanawe ili awe mpatanishi.

Biblia inasema *“Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo*. ***Waefeso 2:13.*** Alimtoa mwanawe wa pekee ili awe mpatanishi na kuondoa kile kizuizi cha dhambi maishani mwako. Bwana Yesu amefanyika kuwa daraja la wewe kukutana na Mungu kwa kubomoa kiambaza.

Wewe usingeweza kujipatanisha mwenyewe au kujiokoa mwenyewe. Yesu pekee ndiye njia, kweli na uzima. Mwanadamu kwa juhudi zake hawezi kuuvuka ule umbali. Ndio maana ilimhitaji Yesu awe daraja. Yeye mwenyewe alisema, *“Mimi ndimi njia, na kweli na uzima. Mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.”* ***Yohana 14:6.*** Hakuna wokovu katika mwingine awaye yote. Kwa maana Jina la Yesu ndilo jina pekee tulilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo. ***Matendo 4:12.*** Ukiamini na kutii, Mungu atafanya makao ndani yako leo.

Hii ni ahadi ya Mungu na ya ajabu. Hataki tu muwe na mahusiano ya kawaida, ila anataka kuishi ndani yako. Yesu alisema, “*Mtu akinipenda atalishika neno langu, na Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake.”* ***Yohana 14:23.***
Unapomkubali Yesu, Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu, wote wanakuja na kugeuza moyo wako kuwa maskani yao ya kudumu. Ni upendo wa ajabu!. Biblia inatuhakikishia kwamba; “*Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote*.”
***1Yohana 1:9.***

Mungu yuko tayari kukupokea na kukufanya uwe kiumbe kipya kama ukimtii na ukimtafuta kwa moyo wako wote. ***Yeremia 29:13.*** Ndugu yangu mpendwa, anza leo maisha mapya na Yesu kwa kutamka sala hii kwa imani;

***Mungu Baba katika jina la Yesu Kristo, nakuja mbele zako kwa shukrani, nikitambua upendo wako kwangu kwa kumtoa mwanao wa pekee, ili afanyike dhabihu ya dhambi zangu na kuondoa lile pazia lililonitenga nawe. Ninatubu dhambi zangu zote na kumpinga shetani katika maisha yangu. Natamka kwa kinywa changu kuwa Yesu Kristo ni Bwana na mwokozi wa maisha yangu. Bwana Yesu, naomba uje ufanye makao ndani yangu pamoja na Mungu Baba na Mungu Roho Mtakatifu. Nielekeze kwenye kweli yote na unipe ujasiri wa kuandamana nawe kila siku za maisha yangu. Asante kwa kunifanya kuwa kiumbe kipya, ninaomba na kuamini katika jina la Yesu, Amen.***